



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEUZI WA MADIWANI
WANAWAKE WA VITI MAALUM**

Dodoma, 28 Januari, 2022

Kwa mujibu wa kifungu cha cha 86A cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Tume ya Taifa ya Uchaguzi katika kikao chake kilichofanyika leo tarehe 28 Januari, mwaka huu imefanya uteuzi wa Madiwani Wanawake wa Viti Maalum watano kujaza nafasi zilizoachwa wazi za Madiwani katika Halmashauri mbalimbali za Tanzania Bara.

Tume imefanya uteuzi huo, baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa, ambaye kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 13 (1) (a) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 aliitaarifu Tume juu ya uwepo wa nafasi wazi za Madiwani Wanawake wa Viti wa Maalum kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), baada ya walioteuliwa awali, kufariki dunia na mwingine kupoteza sifa.

Madiwani Wanawake wa Viti Maalum walioteuliwa ni kama ifuatavyo:-

NA	JINA	HALMASHAURI
1	Cintya Felix Mwalunde	Halmashauri ya Wilaya ya Songwe
2	Amina Alli Kea	Halmashauri ya Wilaya ya Muheza
3	Theresia Peter Mushi	Halmashauri ya Manispaa ya Moshi
4	Leah Constantin Mbilinyi	Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa
5	Amina Ramadhani Mweri	Halmashauri ya Wilaya ya Singida

Imetolewa na:

Gerald G. J. Mwanilwa

KAIMU MKURUGENZILWA UCHAGUZI